

Je, unaishi Korogocho?

Shirikisho la APHRC linalenga kutoa huduma ya afya ya hali ya juu, inayopatikana kwa karibu na iliyo ya bei nafuu na inayolingana na jinsi hali ilivyo mtaa wa Korogocho.

Kupitia mradi huu wa PAMANECH, tunaimarisha huduma za afya kwa akina mama, watoto wachanga na watoto walio chini ya umri wa miaka mitano mtaani Korogocho kupitia njia zifuatazo:

1. Uimarishaji wa mijengo katika vituo vitatu vya kujifungua akina mama visivyo vya kifaida - Provide International, Jamii Kipawa na Mwangaza Ulio na Tumaini
2. Kununua vifaa vya afya kwa vituo hivi
3. Mafunzo kwa wahudumu wa afya katika vituo hivi vitatu
4. Kuwezesha wahudumu wa kiafya wa kijamii (CHVs) kuwatembelea akina mama na watoto manyumbani mwao
5. Usafiri wa kidharura na matibabu ya rufaa

Washikadau na Wanaonufaika

Mradi wa PAMANECH unafanya mtaa wa Korogocho ulioko sub-County ya Kasarani ukishirikiana na Kaunti ya mji wa Nairobi, Timu inayosimamia afya katika Kaunti ndogo ya Kasarani katika wizara ya Afya, Viongozi wa jamii, Wahudumu wa afya wakibinafsi, Vikundi halali vya vijana, Wahudumu wa afya wa kijamii (CHVs) na akina mama na watoto walio chini ya umri wa miaka mitano.

Pata Huduma ya Afya Iliyo ya Hali ya Juu Karibu na Wewe

Tembelea vituo vya Provide International, Jamii Kipawa na Tumaini ambavyo vimeimarishwa kwa hali ya vifaa vya kuwawezesha kutoa huduma ya afya ya hali ya juu kwa akina mama, watoto wachanga na watoto wadogo.

Huduma unazoweza kupata katika hivi vitu 3 ni:

- Huduma ya afya kwa akina mama na watoto wao
- Chanjo
- Huduma kwa akina mama waja wazito
- Huduma kwa akina mama wiki chache baada ya kujifungua
- Huduma za upangaji uzazi
- Huduma ya afya isiyo ya kulazwa
- Kupata ushauri wa muuguzi
- Kumaliza maambukizi ya virusi vya HIV kwa watoto kupitia kina mama waja wazito
- Huduma za maabara
- Huduma za duka za madawa

Tumia Ambulansi ya Dharura kwa Gharama Iliyopunguzwa

Sasa kunapatikana ambulansi ya kuwasafirisha wagonjwa kukiwa na hali ya dharura ya kiafya kwa akina mama waja wazito na watoto wadogo hapa Korogocho. Gharama kwa matumizi ya ambulansi hii imepunguzwa - hii ni kuhakikisha mara ingine ukihataji huduma hiyo usije ukakosa.

Je, wewe ni mja mzito au una mtoto mgonjwa na ungependa kufika Provide International, Jamii Kipawa au Tumaini nyakati za usiku? Pigia simu mhudumu wa afya wa kijamii (CHV) aliye kijijini kwako ama moja ya vikundi tisa vya vijana vilivyoorodheshwa hapa chini. Watakusaidia kufika kituoni.

Hivi vikundi vya vijana na wahudumu wa kiafya wa kijamii wanafanya kazi pamoja kupatiana usalama kwa akina mama waja wazito na watoto wachanga wanaohitaji matibabu nyakati za usiku.

NAME	Village
Mzinduko Self Help Group	Korogocho A
Umoja Youth Group	Korogocho B
Highridge Development Group	Highridge
Rays of Hope Self Help Group	Gitathuru
Towers of Hope Group	Grogan A
Bahatika Self Help Group	Grogan B
Bidii Yetu Youth Group	Kisumu Ndogo
Nyoda Initiatives	Nyayo
Peculiar Youth Group	Ngomongo

Shirikiana na wahudumu wa afya wa kijamii wa Korogocho

Mradi wa PAMANECH umechangia uundaji vyema uundaji vyema wa vikundi tisa vya katika mtaa wa Korogocho

- Umetoa mafunzo kwa wahudumu 180 wa afya wa kijamii
- Wahudumu 90 wa afya wa kijamii wanaofanya kazi na mradi wa PAMANECH wamepewa vifaa vya kazi - Shirikiana nao wanapokutembelea nyumbani kwako – Jukumu lao ni kufuatilia hali ya afya ya akina mama na watoto katika jamii hii.

Je, wewe ni mja mzito au mke/mpenzi wako ni mja mzito?

- Pata huduma kwa walio waja wazito katika vituo vya afya vya Provide International, Jamii Kipawa na Tumaini
- Jifungue katika vituo hivi vilivyoimarisha na kupewa vifaa vya huduma za kuzalisha
- Nyonyeshe mtoto wako mara tu anapozaliwa
- Endea uchunguzi wa kiafya baada ya kujifungua kufanyiwa kuambatana na ushauri wa mhudumu wa afya wa kijamii katika vituo hivi.

Je, una watoto walio chini ya miaka mitano?

- Wapeleke kwa chanjo Provide International, Jamii Kipawa and Tumaini
- Wapeleke wafanyiwe uchunguzi wa kiafya kuthibitisha kama wakuwa vizuri kuambatana na ushauri wa wahudumu wa afya wa kijamii
- Wakiwa na joto au kikohozi au wanaendesha, wapeleke kwa matibabu



Ukiwa na maswali yeyote kuhusu PAMANECH, tafadhali wasiliana na wana kamati inayosimamia mradi huu katika jamii ya Korogocho

APHRC Campus, Manga Close, Off Kirawa Road
P.O. Box 10787-00100, Nairobi, Kenya
Tel: +254 (20) 400 1000 Email: info@aphrc.org
Website: <http://www.aphrc.org>

KILA MAMA NA MTOTO NI WA THAMANA



African Population and
Health Research Center

